



## Penye Wazee hapaharibiki neno: Mazoezi

### Zoezi la 1: Toa maana ya maneno haya

- i) Kuchambua
- ii) Kukomaa
- iii) Kuringa
- iv) Kujisitiri
- v) Kukosea
- vi) Kuachana
- vii) Njama
- viii) kubanana
- ix) Kuwika
- x) Kujionea

### Zoezi la 2: Tungia Sentensi maneno hayo

### Zoezi la 3: Jibu maswali haya

- i) Joe anayezungumziwa alifanya nini?
- ii) Kwanini wanawake wale walikuwa wanaongea vibaya juu ya mke wa Joe?
- iii) Waliona kosa lake hasa ni lipi?
- iv) Kanga alizovaa mke mpa ziliandikwa nini?
- v) Unafikiri maneno ya kanga hizo yanaweza kuwa na maana gani?

### Zoezi la 4: Jibu kweli au Si kweli

- i) Joe alikuwa kapera kwa muda mrefu
- ii) Wanawake majirani
- iii) Mke wa Joe alitoka kijijini
- iv) Wanawake majirani walikuwa na wivu
- v) Joe aliwaliza wanawake kwanini wanamcheka mke wake
- vi) Bi Kizee aliwasaidia kuamua ugomvi

- vii) Jirani za Joe walikuwa wachokozi
- viii) Jirani za Joe walitakiwa kumkaribisha mke wa joe
- ix) Jirani wa Joe walichambua mboga huku wakisema wapiti njia
- x) Methali ya penye wazee huelezea busara ya wazee

### **Zoezi la 5: Kutoa Maana**

Elezea maana ya methali hii “jogoo la shamba haliwiki mjini” kama ilivyotumika katika hadithi hii.

### **Zoezi la 6: Kuandika Muhtasari**

Andika Muhtasari wa igizo hili kama unamwadithia mtu mwingine.

### **Zoezi la 7: Jibu swali hili**

Sikiliza wimbo wa mwanameka uliopigwa na Marijani Rajabu  
[www.youtube.com/watch?v=jjmmjgrSBDY](http://www.youtube.com/watch?v=jjmmjgrSBDY) - wimbo huu unafanana vipi na methali hii?

### **Zoezi la 8: Jibu swali hili**

Taja methali au msemu wa Kiingereza unayofanana na methali hii  
Unaweza kuelezea methali hiyo hutumikaje?

### **Zoezi la 9: Jibu Swali**

Andika kisa kifupi kingine kuelezea methali “Penye wazee hapaharibiki neno

### **Zoezi la 10: Jibu Swali**

Jaribu kuigiza methali hii ili kufanya mazoezi